UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **1 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

MANENO MUHIMU:
Msaada wa Kifedha, Matatizo ya Kifedha, Idhini ya Hali ya Kifedha, Bima ya Matibabu

LENGO/USULI:
Madhumuni ya taarifa ya sera ifuatayo ni kutoa maelezo kuhusu mchakato wa kuwasilisha ombi la msaada wa kifedha, jinsi maombi yanavyopitiwa na namna ambavyo maamuzi ya ustahiki hufanywa, vigezo vya ustahiki wa mipango ya msaada wa kifedha, (ikiwa ni pamoja na ustahiki wa kudhaniwa kabla ya uamuzi wa ustahiki kamili na msaada kwa ajili ya matatizo ya kifedha), kutoa idhini ya hali ya kifedha kwa wagonjwa wenye mahitaji maalum ya matibabu au ya kihisani, jinsi UMMS hujulisha wagonjwa kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha, mchakato wa kukata rufaa, na hatua zisizo za kawaida za kukusanya madeni.

MATUMIZI:
Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote, wauzaji, na mawakala [wafanyikazi wa kujitolea, wahudumu wa matibabu] wa shirika lolote kati ya mashirika yafuatayo yaliyo wanachama wa Mfumo wa Matibabu wa Chuo Kikuu cha Maryland:

- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMMC)
- Kampasi ya Midtown ya Chuo Kikuu cha Maryland (MTC)
- Taasisi ya Marekebisho na Matibabu ya Mifupa na Misuli ya Chuo Kikuu cha Maryland (UMROI)
- Kituo cha Matibabu cha UM cha St. Joseph (UMSJMC)
- Kituo cha Matibabu cha Baltimore Washington cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMBWMC)
- Kituo cha Matibabu cha Eneo la Pwani cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMSRH)
- Kituo cha Matibabu cha Pwani cha Chuo Kikuu cha Maryland katika Dorchester (UMSMCD)
- Kituo cha Matibabu cha Pwani cha Chuo Kikuu cha Maryland katika Easton (UMSME)
- Kituo cha Matibabu cha Mkoa cha Charles cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMCRMC)
- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland cha Upper Chesapeake (UCHS)
- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland cha Mkoa wa Capital (UMCRH)
- Mtandao wa Madaktari wa Chuo Kikuu cha Maryland (UMPN)
- Duka la Dawa la Wagonjwa Wasio wa Kulazwa la UMMS lililoko Weinberg
- Duka la Dawa la UMMC la Redwood
- Huduma za Maduka ya Dawa za UMMS
- Duka la Dawa la Kampasi ya UMMC ya Mid-Town
- Duka la Dawa la UMMC la Eneo la Capital
- Duka la Dawa la UMMC la Baltimore Washington

FAFANUZI:

Kiwango cha Umaskini cha Serikali ya Taifa	Hiki ni kipimo cha mapato kinachotolewa kila mwaka na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu (HHS). Viwango vya umaskini vya serikali ya taifa hutumiwa ili kuamua ustahiki wa mipango na mafao fulani.
Matatizo ya Kifedha	Visa ambapo gharama za mashirika yaliyo wanachama ambazo zilipatikana katika mashirika yaliyo wanachama wa UMMS kwa ajili ya huduma za utambuzi wa magonjwa au kutibu maradhi na majeraha kwa ajili ya kaya kwa muda wa miezi kumi na miwili (12) ambazo zimepita 25% ya mapato ya mwaka ya kaya hiyo.

UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **2 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

Vikomo vya MDH	Ni vikomo vya ustahiki kulingana na mapato kwa ajili ya matibabu yenye bei iliyopunguzwa ambavyo vimewekwa na ofisi ya Mipango ya Bima ya Matibabu ya Idara ya Afya ya Maryland (MDH. Jimbo la Maryland lilikubali upanuzi wa Medicaid wa Serikali ya Taifa mnamo Januari 1, 2014, dhidi ya viwango vya Umaskini vya Serikali ya Taifa, chini ya Sheria ya Matibabu ya Bei Nafuu, ambayo ilipanua vikomo vya ustahiki kulingana na mapato vya mpango wa Medicaid wa Maryland. UMMS ilianza kutumia vikomo hivi vipya kwa ajili ya gharama za matibabu zinazopunguzwa kulingana na mapato, kama ilivyoelezwa kwenye Kiambatisho cha A.
Deni Linalotokana na Huduma za Matibabu	Gharama za kujilipia kwa pesa zako mwenyewe, ikiwa ni pamoja na kiasi cha malipo, bima na makato iliyotokea katika shirika la wanachama wa UMMS kwa sababu ya huduma muhimu ya kiafya.
Ustahiki wa Kudhaniwa	Visa ambapo taarifa zilizotolewa na mgonjwa au kupitia vyanzo vingine zinatoa ithibati tosha kwamba mgonjwa huyo anastahiki kupokea msaada wa kifedha, ila hakuna fomu ya kuomba msaada wa kifedha katika faili.

SERA:
University of Maryland Medical System ("UMMS") imejitolea kutoa msaada wa kifedha kwa watu walio na mahitaji ya huduma za afya na wasio na bima, wasio na bima kamili, wasiostahiki kwa mipango ya serikali, au kwa sababu zingine wasioweza kulipia matibabu ya magonjwa yanayojitokeza na yanayohitaji matibabu, kulingana na hali zao binafsi za kifedha.

Ni sera ya mashirika yaliyo wanachama wa Mfumo wa Matibabu wa Chuo Kikuu cha Maryland (“UMMS”) kutoa usaidizi wa kifedha ambayo inaambatana au kupita vigezo vilivyo wekwa na jimbo la Maryland kwa wagonjwa walio na hali hiyo ya kifedha.

I. **Matibabu Bila Malipo -** Watu walio na mapato ya kiasi cha hadi asilimia 200 ya vikomo vya ustahiki vya mapato vilivyowekwa na Idara ya Afya ya Maryland wanastahiki kupata matibabu bila malipo.
II. **Matibabu kwa Bei Zilizopunguzwa -** Watu walio na kati ya asilimia 200 hadi 300 ya vikomo vya ustahiki vya mapato vilivyowekwa na Idara ya Afya ya Maryland wanastahiki kupokea mapunguzo kwa kuzingatia gharama zinazobadilika kulingana na mapato, kama ilivyoelezwa kwenye Kiambatisho cha A.
III. **Matatizo ya Kifedha -** Watu wasiostahiki kupata msaada wa kifedha chini ya miongozo ya msingi ya sera hii, lakini wana madeni ya huduma za matibabu yaliyotokana na kupokea huduma katika mashirika yaliyo wanachama wa UMMS ambayo yamezidi asilimia 25 ya Mapata ya Mwaka ya Kaya, wanastahiki kupata msaada kwa ajili ya matatizo ya kifedha.

Mipango ya kufanya malipo pia inapatikana kwa wagonjwa wote. Masharti ya mipango hiyo yanaweza kurekebishwa kufuatia ombi la mgonjwa. Taarifa za ziada kuhusu mipango ya kufanya malipo zinapatikana katika Sera ya Mipango ya Malipo ya UMMS. Ni haki ya UMMS kufanya uamuzi kwa hiari yake kuhusu uwezo wa mgonjwa kuweza kulipa. Wagonjwa wote wanaotafuta huduma za dharura watahudumiwa bila kujali uwezo wao wa kulipa. Ili kupata huduma kwa matatizo yanayohitaji matibabu ya dharura/ya hapohapo, maombi

ya msaada wa kifedha yatakamilishwa, kupokelewa na kufanyiwa utathmini kwa kuzingatia Hata hivyo, taratibu hizo hazitazuia wagonjwa kupata matibabu.

UTARATIBU:

I. Jinsi ya Kuwasilisha Ombi la Msaada wa Kifedha

Kwa kipindi chochote cha matibabu, mchakato wa kuwasilisha maombi ya msaada wa kifedha utafunguliwa kwa angalau siku 240 baada ya bili ya kwanza kutumwa baada ya mgonjwa kuruhusiwa kuondoka hospitalini. Kwa hiari yao, wagonjwa wanaweza kuomba msaada wa kifedha kabla au baada ya kupokea huduma za matibabu, au wanaweza kutambuliwa kama wanaoweza kupata msaada wa kifedha wakati wa mchakato wa kutoa idhini ya hali ya kifedha au katika uchunguzi wa ustahiki wa kudhaniwa wa kupata msaada wa kifedha.

Kutoa idhini ya hali ya kifedha ni mchakato unaobaini uwezo na uwezekano wa mgonjwa wa kulipa. Inapowezekana, juhudi zitafanywa ili kutoa idhini ya hali ya kifedha kabla ya tarehe ya huduma. Wakati wa mchakato wa kutoa idhini ya hali ya kifedha, wagonjwa watakaoonyesha kwamba hawana ajira wala bima watatakiwa kuwasilisha maombi ya msaada wa kifedha kabla ya kupata huduma za matibabu yasiyo ya dharura (isipokuwa kama wanatimiza vigezo vya ustahiki wa kudhaniwa wa kupata msaada wa kifedha kabla ya kupata ustahiki kamili).

Kutakuwa na mchakato mmoja wa maombi kwa mashirika yote ambayo ni wanachama wa UMMS. Mpango wa Msaada wa Fedha utakubali Daktari wa Kitivo, Inc's (FPI) kukamilika kwa maombi ya msaada wa kifedha katika kuamua kustahiki mpango wa UMMS wa Msaada wa Kifedha. Wagonjwa wanahitajika kuwasilisha ombi lililokamilishwa la msaada wa kifedha (lililo na taarifa na hati zote zinazohitajika), isipokuwa kama wanatimiza vigezo vya ustahiki wa kudhaniwa. Ili kuwezesha mchakato huu, kila anayetuma ombi lazima atoe maelezo kuhusu ukubwa na mapato ya familia yake. Kuwasilishwa maelezo yanayohitajika kwa njia ya mdomo kutakubaliwa, panapotumika.. UMMS itatoa fomu za maombi ya msaada wa kifedha kwa wagonjwa wote bila kujali hali yao ya bima ya afya, ikiwa ni pamoja na wagonjwa wasio na bima, na fomu za maombi zitapatikana wakati wowote kwenye tovuti ya UMMS na pia zitatolewa kwa watakaoziomba.

<u>Hati Zinazohitajika kwa Ajili ya Maombi ya Msaada wa Kifedha</u>

Ili kuwasaidia waombaji kukamilisha mchakato wa maombi, hati zinazohitajika na zinazopendekezwa zitaorodheshwa vyema kwenye fomu ya kuwasilisha ombi la msaada wa kifedha, ikiwa ni pamoja na:

- Nakala ya hivi karibuni zaidi ya matangazo ya kodi ya mapato (kama una mume/mke na hamtangazi kodi kwa pamoja, ambatisha nakala ya matangazo ya mume/mke wako); thibitisho la mapato ya ulemavu (kama inahitajika) thibitisho la mapato ya usalama wa kijamii (kama inahitajika).
- Ikiwa huna ajira, ithibati tosha ya kukosa ajira kama vile taarifa kutoka Ofisi ya Bima ya Wasio na Ajira, taarifa kutoka kwa mfadhili wa hivi sasa, n.k.
- Nakala ya hivi karibuni zaidi ya hati ya malipo (kama umeajiriwa) au ithibati nyingine ya mapato.
- Taarifa ya Uamuzi Kuhusu Bima ya Matibabu (kama inahitajika).
- Nakala za bili ya Rehani au Kodi ya nyumba (kama inahitajika), au nyaraka iliyoandikwa kuhusu hali yako ya sasa ya nyumba/makazi.

- Ikiwa mgonjwa atawasilisha nakala zote za matangazo ya kodi ya mapato na nakala ya mishahara yao ya hivi karibuni (au thibitisho nyingine ya mapato), na hati moja tu kati ya hizo mbili zinaonyesha kustahiki msaada wa kifedha, hati ya hivi karibuni itaamua ustahiki.

Msaada wa kifedha huenda usikataliwe kulingana na kutotoa taarifa au hati ambazo hazihitajiki kulingana na sera hii au kulingana na fomu za kuomba msaada wa kifedha, na UMMS ina haki kamili ya kutoa msaada wa kifedha kwa wagonjwa ambao hawajawasilisha hati zote zinazohitajika.

- Ikiwa mgonjwa atawasilisha ombi la msaada wa kifedha bila taarifa au hati zinazohitajika ili kufanya uamuzi wa mwisho wa ustahiki, ombi la maandishi la kuomba taarifa au hati hizo ambazo hazikutolewa litatumwa kwa mgonjwa.
- Ombi hili la maandishi pia litakuwa na maelezo ya mawasiliano (ikiwa ni pamoja na nambari ya simu na anwani ya ofisi) ya ofisi au idara ambayo inaweza kutoa taarifa kuhusu msaada wa kifedha na usaidizi wa mchakato wa kuwasilisha maombi.
- Mgonjwa atakuwa na siku thelathini (30) kutoka tarehe ambayo ombi hili la maandishi litatolewa ili awasilishe taarifa au hati zinazohitajika ili ombi lake la ustahiki lishughulikiwe. Ikiwa hakuna taarifa zitakazopokelewa ndani ya siku 30, barua itatumwa ili kumjulisha mgonjwa kwamba ombi lake sasa limetamatishwa kwa sababu ya ukosefu wa hati zinazohitajika.
- Mgonjwa anaweza kuwasilisha ombi la msaada wa kifedha upya na kuanzisha mchakato mpya wa ombi kwa kuwasilisha taarifa au hati ambazo hazikuwepo

II. Kupitia na Kubaini Ustahiki wa Maombi ya Msaada wa Kifedha

Kuna wafanyakazi walioteuliwa ambao watakuwa na wajibu wa kupokea maombi ya misaada ya kifedha. Wafanyakazi hao wanaweza kuwa washauri wa masuala ya kifedha, waratibu wa fedha ambazo bado hazijalipwa kwa ajili ya huduma ambazo mgonjwa tayari amepokea, au wakala za mhusika wa tatu zinazofanya kazi kama nyongeza ya ofisi kuu ya kazi. Ili kusaidia waombaji kukamilisha mchakato huo, UMMS itatoa fomu za kuwasilisha maombi ya msaada wa kifedha ambazo zitawajulisha kuhusu hati zinazohitajika ili kufanya maamuzi ya mwisho ya ustahiki. Inapowezekana, wafanyakazi walioteuliwa watashauriana na wagonjwa waliotuma maombi ya misaada ya kifedha kupitia simu au kukutana na wagonjwa hao ili kubaini kama wanatimiza vigezo vya msingi vya kupata msaada.

Data za mwanzo zitawekwa katika mfumo wa ubadilishanaji data wa mhusika wa tatu ili kuwawezesha wafanyakazi walioteuliwa kufuatilia maombi na kubaini ustahiki wa kupata msaada wa kifedha. Wafanyakazi walioteuliwa watakuwa na majukumu yafuatayo:

- Kubaini ikiwa mgonjwa huyo ana bima ya afya. Wagonjwa ambao wana bima nyingine ya matibabu (kwa mfano, bima ya msingi na ya sekondari au mtoa huduma anayehitajika), lazima watumie na kumaliza mafao ya mtandao wao kabla ya kutuma ombi la kupata msaada wa kifedha.
- Ikiwa mgonjwa anastahiki kupata bima ya COBRA, uwezo wa kifedha wa mgonjwa huyo wa kulipia malipo ya bima utakaguliwa na mfanyakazi aliyeteuliwa na mapendekezo yatatolewa kwa Viongozi Wakuu.
- Kukamilisha uchunguzi wa ustahiki kwenye mpango wa Medicaid wa wagonjwa Wanaolipia Gharama Zao Wenyewe ili kuthibitisha ikiwa mgonjwa ana bima katika wakati huo. Ili kuwezesha mchakato huu, kila anayetuma ombi lazima atoe maelezo kuhusu ukubwa wa familia yake na mapato.

- Kubaini ikiwa mgonjwa ana ustahiki wa kudhaniwa ili aweze kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa.
- Kubaini ikiwa wagonjwa wasio na bima wanastahiki kupata bima ya afya ya umma au binafsi. Watu walio na uwezo wa kifedha wa kulipia bima za afya watahimizwa kufanya hivyo, kama njia ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya, na kwa ajili ya afya yao binafsi kwa jumla.

Kwa kiwango kinachowezekana, wafanyakazi walioteuliwa watatoa usaidizi kwa wagonjwa wasio na bima ikiwa mgonjwa atachagua kuwasilisha ombi la kupata bima ya afya ya umma au binafsi, kubaini ikiwa mgonjwa huyo anastahiki kwa mipango mingine ya umma ambayo inaweza kumsaidia kulipa gharama za matibabu, na kutumia taarifa ambazo UMMS inazo ili kubaini ikiwa mgonjwa huyo anastahiki kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa hini ya sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS.

Ndani ya siku mbili za kazi baada ya kupokelewa kwa ombi la mgonjwa la msaada wa kifedha au ombi la bima ya matibabu, UMMS lazima itoe uamuzi wa uwezekano wa kupata ustahiki. Uamuzi wa ustahiki wa muda kabla ya kubainishwa kwa ustahiki kamili unaweza kubadilika, kwa kuzingatia hati za ombi zilizopokelewa.

Ikiwa ombi la mgonjwa la msaada wa kifedha limebainika kuwa kamili na sahihi, mfanyakazi aliyeteuliwa atapendekeza kiwango cha ustahiki cha mgonjwa huyo na kuwasilisha ombi la kupata idhini ya pili na ya mwisho. UMMS itatoa uamuzi wa mwisho wa ustahiki wa mgonjwa ndani ya siku 14 baada ya mgonjwa huyo kuwasilisha ombi lililokamilishwa la msaada wa kifedha na kusimamisha shughuli zozote za kutuma bili za gharama au hatua za kukusanya madeni huku uamuzi wa ustahiki ukifanywa.

Ikiwa Ombi la Msaada wa Kifedha Litaidhinishwa

Mara baada ya mgonjwa kuidhinishwa kupokea msaada wa kifedha, bima ya msaada wa kifedha hutumika katika mwezi wa uamuzi huo, na mwaka mmoja kabla ya uamuzi huo.

- Barua ya uamuzi wa mwisho itawasilishwa kwa kila mgonjwa ambaye amewasilisha ombi rasmi la msaada wa kifedha, ikiwa ni pamoja na (kama inatumika): msaada ambao mgonjwa huyo anastahiki kupokea na msingi wa uamuzi huo.
- Shirika la UMMS linaweza kuongeza kipindi cha ustahiki wa kupata msaada wa kifedha kwa kuongeza muda kwa siku zilizopita au siku za usoni kulingana na hali ya kila ombi.
- Msaada wa kifedha kwa kawaida hutumika kwa matibabu yote ya dharura na huduma zingine zinazohitajika kutambua dalili au kutibu magonjwa na majeraha ambazo zinatolewa na kila shirika lililo mwanachama wa UMMS (Tazama Hali Zisizotumika ili kupata maelezo zaidi).
- Ikiwa huduma za ziada za matibabu zitatolewa baada ya kipindi cha ustahiki, sharti wagonjwa wawasilishe upya ombi la msaada wa kifedha.
- Ikiwa itabainishwa kwamba mgonjwa anastahiki kupata matibabu kwa gharama iliyopunguzwa, na tayari amepokea taarifa ya huduma za matibabu anazostahiki kupokea katika kipindi cha bima ya msaada wa kifedha, mgonjwa huyo pia atapokea bili inayoonyesha kiwango ambacho anadaiwa kwa ajili ya matibabu baada ya kutumika kwa msaada wa kifedha.
- Ikiwa mgonjwa amelipia huduma za matibabu kabla ya kuidhinishwa kupokea msaada wa kifedha, huenda akastahiki kurudishiwa pesa. Maamuzi ya kurejesha pesa hulingana na wakati ambapo ilibainishwa kwamba mgonjwa hangeweza kulipa ikilinganishwa na wakati ambapo malipo ya mgonjwa huyo yalifanywa. Ikiwa kiasi kilichobainishwa kama ambacho mgonjwa anaweza kulipa kiko chini ya

kiasi anachohitajika kulipa, salio lililopo litarejeshwa kwa mgonjwa ikiwa kiasi hicho kinazidi kiasi kilichobainishwa kama ambacho mgonjwa anaweza kulipa kwa $5.00 au zaidi. Hii ni pamoja na maamuzi ya ustahiki wa kupokea msaada wa kifedha ndani ya siku 240 baada ya bili ya kwanza kutolewa.

Ikiwa kuna mabadiliko katika mapato ya mgonjwa, mali, gharama, au hali ya familia, mgonjwa anatarajiwa kujulisha Idara ya Msaada wa Kifedha kuhusu mabadiliko hayo kupitia 410-821-4140. Ili kuwezesha mchakato huu, na kuhakikisha kwamba wagonjwa wana fursa ya kutathminiwa upya kwa ajili ya ustahiki wa msaada wa kifedha ndani ya siku 240 baada ya bili ya kwanza, UMMS itajulisha wagonjwa kwamba ikiwa mapato yao yamebadilika, wanafaa kuwasiliana na Idara ya Mpango wa Msaada wa Kifedha kuhusu kila bili.

Ikiwa Ombi la Msaada wa Kifedha Halitaidhinishwa

Ikiwa itabainiwa kwamba mgonjwa hastahiki kupata msaada wa kifedha kabla ya kupokea huduma (kwa ajili ya huduma hiyo), hatua zote za kutoza kiasi cha pesa kinacholipwa kwa mhudumu ili kupokea huduma za bima, kiasi unacholipia bima ili ianze kutumika, au asilimia fulani ya salio linalotarajiwa kwa ajili ya huduma hiyo zitafanywa kabla ya tarehe ya huduma au huenda pesa hizo zikaratibiwa kukusanywa katika tarehe hiyo ya huduma.

- Ikiwa itabainiwa kwamba mgonjwa hastahiki kupata msaada wa kifedha, na alikuwa amewasilisha ombi la kupata idhini ya hali ya kifedha kwa ajili ya huduma zisizo za dharura au huduma zisizohitaji matibabu ya hapohapo katika hospitali, mfanyakazi aliyeteuliwa atamjulisha daktari kuhusu uamuzi huo na uduma zisizo za dharura au huduma zisizohitaji matibabu ya hapohapo katika hospitali hazitaratibiwa.
- Daktari anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu na kuomba uamuzi mbadala kutoka kwa Kamati Tendaji ya Kutoa Idhini ya Hali ya Kifedha kwa kuzingatia kila kesi.
- Kwa huduma zisizo za dharura au huduma zisizohitaji matibabu ya hapohapo, maombi ya msaada wa kifedha yatakamilishwa, kupokelewa, na kutathminiwa kuanzia siku za awali na mchakato huu hautachelewesha wagonjwa kupokea matibabu.
- Wagonjwa wasiostahiki kupata msaada wa kifedha watatakiwa kulipa masalio yoyote ya gharama yaliyopo na huenda wakawasilishwa kwa huduma ya kukusanya madeni yasiyotarajiwa kulipwa ikiwa masalio hayo hayatalipwa katika wakati uliokubaliwa.
- Mgonjwa anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi, tafadhali tazama sehemu ya Rufaa kwa maelezo zaidi.
- Kwa kipindi chochote cha matibabu, mchakato wa kuwasilisha maombi ya msaada wa kifedha utafunguliwa kwa angalau siku 240 baada ya bili ya kwanza kutumwa baada ya mgonjwa kuruhusiwa kuondoka hospitalini.

III. Vigezo vya Ustahiki

UMMS itatoa msaada wa kifedha wakati mapitio ya hali ya kifedha ya mgonjwa binafsi yamefanywa na kunakiliwa. UMMS haitatumia uraia au hali ya uhamiaji ya mgonjwa kama hitaji la kubaini ustahiki wa msaada wa kifedha; au kumnyima msaada wa kifedha au kukataa ombi la msaada wa kifedha la mgonjwa kwa msingi wa mbari, rangi, dini, asili au nchi anayotoka, jinsia, umri, hali ya ndoa, mwelekeo wa kimapenzi, jinsia ambayo mtu anajitambulisha nayo, maelezo ya kijeni, au kwa msingi wa ulemavu.

UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **7 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

Vigezo vifuatavyo vitatumika katika kutathmini ustahiki wa mgonjwa wa kupata msaada wa kifedha, ustahiki wa kudhaniwa kwa ajili ya maombi ya msaada wa kifedha, na ustahiki wa maombi ya msaada wa matatizo ya kifedha.

Ustahiki wa Kupata Msaada wa Kifedha

UMMS itazingatia vikomo vya mapato ya kaya vya MDH ili kubaini ustahiki wa msaada wa kifedha na kiwango cha matibabu bila malipo au yaliyopunguzwa gharama ambayo yatatolewa kwa wagonjwa wanaostahiki. UMMS itatathmini mapato ya familia (kaya) ya mgonjwa wakati wa kutolewa kwa huduma. Ili kuzingatia mabadiliko yoyote ya hali ya kifedha, UMMS itatathmini upya mapato ya familia (kaya) ndani ya siku 240 baada ya bili ya kwanza ya hospitali kutolewa.

Huenda UMMS ikazingatia rasilimali za kifedha za kaya katika kubaini ustahiki wa kupokea matibabu bila malipo na matibabu yenye gharama iliyopunguzwa chini ya sera ya msaada wa kifedha, kando na vigezo vinavyozingatia mapato. Rasilimali za kifedha zitafanyiwa marekebisho kila mwaka kulingana na kupanda kwa gharama ya maisha kwa mujibu wa Kielezo cha Mabadiliko ya Bei kwa Wateja. Rasilimali zifuatazo za kifedha zinazoweza kufanywa pesa taslimu hazitajumuishwa:

- Kwa kiwango cha chini zaidi, dola 10,000 za kwanza za rasilimali za kifedha.
- Hisa za kiasi cha $150,000 zilizowekezwa katika makazi ya msingi.
- Rasilimali za uzeeni ambazo Huduma ya Ushuru ya Mapato ya Ndani imezipa msamaha wa ushuru kama akaunti ya akiba ya uzeeni, ikiwa ni pamoja na mipango ya fidia kidogo ambayo inastahiki chini ya Kanuni ya Mapato ya Ndani au mipango ya fidia kidogo isiyostahiki.
- Gari moja linalotumika kwa ajili ya mahitaji ya usafiri ya mgonjwa au jamaa mwingine wa mgonjwa huyo;
- Rasilimali zingine zozote ambazo hazikujumuishwa wakati wa kubaini ustahiki wa kifedha chini ya Mpango wa Msaada wa Matibabu chini ya Sheria ya Usalama wa Jamii.
- Fedha zilizolipwa awali kwa ajili ya masomo ya chini zilizo katika akaunti ya Mpango wa Maryland 529.

Katika kubaini mapato ya familia ya mgonjwa, UMMS itatumia ukubwa wa kaya inayojumuisha mgonjwa na, kwa kiwango cha chini zaidi, mume/mke (bila kujali kama mgonjwa na mume/mke wake wanatarajia kutangaza ushuru wa Jimbo kwa pamoja), watoto wa damu, watoto wa kuasili, au watoto wa kambo, na mtu yeyote ambaye mgonjwa huyo anajumuisha katika matangazo yake katika matangazo ya ushuru ya taifa au Jimbo. Kwa mgonjwa ambaye ni mtoto, ukubwa wa kaya utajumuisha mtoto huyo na wazazi wake wa damu, wazazi wa kuasili, au wazazi wa kambo au walezi, ndugu zake wa damu, ndugu wa kuasili, au ndugu wa kambo, pamoja na mtu mwingine yeyote ambaye mzazi au mlezi wa mgonjwa huyo anajumuisha katika matangazo yake katika matangazo ya ushuru ya taifa au Jimbo.

Wagonjwa wanaweza kuchukuliwa kwamba hawastahiki kupata msaada wa kifedha:

- Ikiwa wana bima (k.m., HMO, PPO, Fidia ya Wafanyakazi Waliopata Maradhi/Kujeruhiwa Kazini, Medicaid, au mipango mingine ya bima), ambayo huwanyima huduma za UMMS kutokana na vikwazo/mipaka inayowekwa na mipango hiyo ya bima.
- Ikiwa watakataa kuchunguzwa kwa ajili ya mipango mingine ya msaada kabla ya kuwasilisha ombi la kupokea msaada wa kifedha.

- Ikiwa watakataa kutoa taarifa zinazohusiana na madai ya kesi ya dhima ya kisheria inayoendelea.

Kwa kawaida, msaada wa kifedha hutumika kwa matibabu yote ya dharura na huduma zinazohitajika ili kutambua dalili na kutibu magonjwa na majeraha; hata hivyo, huenda hali zifuatazo zisitumike:

- Huduma zinazotolewa na watoa huduma wa afya wasio na uhusiano na mashirika yaliyo wanachama wa UMMS (k.m, vifaa vya kudumu vya matibabu, huduma za afya zinazotolewa nyumbani).
- Huduma ambazo zimekataliwa na mpango au sera ya bima ya mgonjwa (k.m., HMO, PPO, au Fidia ya Wafanyakazi Waliopata Maradhi au Kujeruhiwa Kazini). Hali zisizotumika zinaweza kubainishwa kulingana na kila hali, kwa kuzingatia athari kwa matibabu na mpango.
- Huduma za mapambo ya mwili au huduma zisizohitajika ili kutambua maradhi au kutibu magonjwa na majeraha.
- Bidhaa ambazo mgonjwa hununua mara kwa mara za matumizi ya kila siku, chakula, na malazi.
- Malazi yenye Usimamizi pamoja na chakula wakati mgonjwa amendikishwa kwenye Mpango wa Mchana.
- Madai ya Dhima ya Mhusika wa Tatu (Ajali za Magari, Fidia ya Wafanyakazi Waliopata Maradhi au Kujeruhiwa Kazini, Majeraha ya Mwili, au dai lingine la kisheria) hadi wakati njia zote za kufanya malipo zimetumika kikamilifu.

Msaada wa kifedha kwa ajili ya ada za huduma za kitaalamu uliotolewa chini ya sera hii hutumika kwa Mtandao wa Madaktari wa UM (UMPN). Wagonjwa ambao wanataka kupata msaada wa kifedha unaohusiana na kulipia ada za huduma zisizotolewa na wataalamu wa Mtandao wa Madaktari wa UM sharti wawasiliane na daktari au mtoa huduma huyo kwa njia ya moja kwa moja. Orodha ya madaktari wanaotoa huduma za matibabu zinazohitajika ili kutambua dalili au kutibu maradhi na majeraha inaweza kupatikana katika tovuti ya kila shirika la UMMS. Orodha hii hutoa maelezo mahususi kuhusu madaktari wasioshiriki katika Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS.

<u>Ustahiki wa Kudhaniwa wa Msaada wa Kifedha</u>

Katika hali ambapo hakuna ithibati ya kuunga mkono ustahiki wa mgonjwa wa kupata msaada wa kifedha, UMMS ina haki kamili ya kubaini ikiwa mgonjwa ana ustahiki wa kudhaniwa wa kupata msaada wa kifedha kwa ajili ya akaunti zote za hospitali. Ili kubaini ustahiki wa kudhaniwa wa kupata msaada wa kifedha, UMMS inaweza kutumia wakala au taarifa za nje ili kukadiria mapato ambayo yanaweza kutumiwa ili kutathmini ustahiki wa mgonjwa wa kupata ustahiki wa msaada wa kifedha. Kwa kuwa ustahiki wa kudhaniwa kwa kawaida huwa wa kudumu, UMMS itatoa matibabu bila malipo kwa wagonjwa waliobainishwa kwamba wana ustahiki wa kudhaniwa wa kupata msaada wa kifedha. Ustahiki wa kudhaniwa wa msaada wa kifedha utatumika tu katika tarehe mahususi ambayo mgonjwa atapokea huduma. Makundi ya wahudumu wa Mtandao wa Madaktari wa UM watatoa msaada wa kifedha wakizingatia salio ambalo halikulipiwa na bima kwa msingi wa uamuzi wa kubaini ustahiki kwa kutumia gharama ya hospitali ambayo haijalipwa na bima.

Ustahiki wa kudhaniwa unaweza kubainishwa kwa msingi wa hali binafsi za mgonjwa ambazo zinaweza kuwa pamoja na:

a. Bima Halali ya Matibabu ya kulipia dawa
b. Bima ya (SLMB) Medicare ya Mapato Mahususi ya Kiwango cha Chini
c. Bima ya (PAC) Matibabu ya Msingi kwa Watu Wazima

d. Kukosa makazi
e. Mgonjwa ana Bima ya Matibabu hivi sasa
f. Wagonjwa walio na Bima ya Matibabu na Wagonjwa Wenye Matibabu Yanayosimamiwa na Medicaid kwa ajili ya huduma zinazotolewa katika chumba cha matibabu ya dharura ambazo hazilipiwi na bima za mipango hii
g. Viwango vya gharama zinazolipiwa kwa mapato ili kustahiki kupata Bima ya Matibabu
h. Kustahiki kwa mipango mingine ya misaada ya jimbo au mtaa, kama vile:
   i) Mpango wa Msaada wa Vyakula vya Kuimarisha Lishe
   ii) Mpango wa Msaada wa Gharama za Kawi wa Jimbo
   iii) Mpango wa Vyakula Maalum vya Kuimarisha Lishe kwa Ajili ya Wanawake, Watoto Wachanga, na Watoto
   iv) Mpango mwingine wowote wa huduma za jamii kama ilivyobainishwa na Idara ya Afya na Afya ya Akili ya Maryland (MD DHMH) na Tume ya Mapitio ya Gharama za Huduma za Afya (HSCRC).
i. Mgonjwa amefariki na hakuna mali yake yoyote inayojulikana
j. Wagonjwa ambao wamebainika kwamba wanatimiza vigezo vya ustahiki vilivyowekwa chini ya Mpango wa awali wa Bima ya Matibabu Unaoendeshwa na Jimbo Pekee
k. Watu wasio raia wa Marekani ambao ilibainishwa kwamba hawastahiki
l. Huduma za Bima ya Matibabu zisizostahiki kwa ajili ya wagonjwa wanaostahiki kupata Bima ya Matibabu
m. Wagonjwa wasiotambulika (Akaunti zisizojulikana na ambazo juhudi zote za kuzipata na/au kuzitambua hazijafaulu)
n. Kufilisika, kwa mujibu wa sheria, kama ilivyowekwa na mahakama ya taifa
o. Ustahiki katika mipango mahususi ya matibabu ya UMMS (ikiwa ni pamoja na: Mpango wa Msaada wa St. Clare, Mpango wa Huduma za Uzazi wa UMMS, Mpango wa Ugonjwa wa Ngiri (UMSJMC).

Wagonjwa wasio na bima waliohudumiwa katika Idara ya Dharura baada ya kuwasilishwa kwa Ombi la Kutathmini Mahitaji ya Huduma za Dharura kwa Mgonjwa hawatazingatiwa ili kupokea msaada wa kifedha kwa ustahiki wa kudhaniwa hadi wakati ambapo mpango wa Medicaid wa Afya ya Akili wa Maryland utakapotumiwa bili.

<u>Ustahiki wa Kupata Msaada kwa Ajili ya Matatizo ya Kifedha</u>

Msaada kwa ajili ya matatizo ya kifedha hupatikana kwa wagonjwa ambao kwa sababu fulani hawastahiki kupata msaada wa kifedha chini ya miongozo ya msingi ya sera hii, lakini wana deni linalotokana na huduma za matibabu zinazohitajika kutambua na kutibu maradhi la kipindi cha miezi kumi na miwili (12) linalozidi asilimia 25 ya mapato ya familia ya mgonjwa.

- Kiasi cha gharama za matibabu zisizolipiwa na bima ambazo zilitokana na huduma za mashirika yote yaliyo wanachama wa UMMS yatazingatiwa wakati wa kubaini ustahiki wa mgonjwa (ikiwa ni pamoja na akaunti zitakazochukuliwa kama madeni yasiyotarajiwa kulipwa, isipokuwa akaunti zilizofunguliwa kesi na hukumu kutolewa) na gharama zozote za matibabu zinazotarajiwa.
- Kwa wagonjwa wanaostahiki kupata matibabu kwa bei iliyopunguzwa chini ya vigezo vya msaada wa kifedha na pia wanatimiza vigezo vya ustahiki wa msaada wa matatizo ya kifedha, UMMS itatoa kiasi cha jumla cha mapunguzo ya ada yanayostahiki.

- Ili kutathmini mapato ya kaya, UMMS itatumia vigezo sawa na vile vilivyo katika sehemu ya Ustahiki wa Msaada wa Kifedha katika sera hii ili kukokotoa mali, mapato ya kaya, na ukubwa wa familia.
- Mara tu mgonjwa anapoidhinishwa kwa msaada wa matatizo ya kifedha, bima itaanza kutumika katika mwezi wa tarehe ya kwanza ya kustahiki kupata huduma na mwaka mmoja kabla ya uamuzi. Shirika la UMMS linaweza kuongeza kipindi cha ustahiki wa kupata msaada wa matatizo ya kifedha kwa kuongeza muda kwa siku zilizopita au siku za usoni kulingana na hali ya kila ombi.
- Msaada kwa ajili ya matatizo ya kifedha utalipia mgonjwa pamoja na wanafamilia wanaostahiki ambao wanaishi katika makazi hayo kwa ajili ya gharama zilizoidhinishwa za matibabu kwa bei iliyopunguzwa pamoja na kipindi cha ustahiki wa matibabu yanayohitajika ili kutambua na kutibu maradhi na wataendelea kustahiki kupata matibabu yanayohitajika ili kutambua na kutibu maradhi kwa bei iliyopunguzwa watakapohitaji huduma baadaye katika shirika lilo hilo lililo mwanachama wa UMMS ndani ya kipindi cha miezi 12 kuanzia tarehe ambayo matibabu yanayohitajika ili kutambua na kutibu maradhi kwa bei iliyopunguzwa yalitolewa kwa mara ya kwanza. Ili kuzuia kurudufiwa kimakosa kwa maamuzi ya UMMS ya ustahiki wa kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa, mgonjwa au wanafamilia wanaostahiki watajulisha UMMS kuhusu ustahiki wa mgonjwa au mwanafamilia wa kupata matibabu yanayohitajika kutambua na kutibu maradha kwa bei iliyopunguzwa.

Hali zingine zote za ustahiki, kutostahiki, na taratibu za vigezo vya ustahiki wa msingi wa kupata msaada wa kifedha zitatumika kwa vigezo vya kupata msaada wa matatizo ya kifedha, isipokuwa katika hali nyingine iliyo hapo juu.

IV. Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi wa Ustahiki wa Msaada wa Kifedha

Wagonjwa ambao maombi yao ya msaada wa kifedha yamekataliwa wanaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Rufaa inaweza kuwasilishwa kwa njia ya mdomo au kwa maandishi. Wagonjwa wanahimizwa kuwasilisha hati zaidi zitakazotoa sababu madhubuti za kubatilishwa kwa uamuzi wa kunyimwa msaada.

Ikiwa mgonjwa angetaka kukata rufaa, UMMS:

- Itajulisha mgonjwa huyo kwamba Kitengo cha Elimu ya Afya na Utetezi kiko tayari kumsaidia yeye au mwakilishi a wake aliyeidhinishwa katika kuwasilisha rufaa na kujaribu kufanya mapatano ya kuomba uamuzi tofauti.
- Kutoa anwani, nambari ya simu, nambari ya faksi, anwani ya barua pepe, anwani ya posta, na tovuti ya Kitengo cha Elimu ya Afya na Utetezi: Office of the Attorney General, Health Education and Advocacy Unit | 200 St. Paul Place, 16th Floor, Baltimore, MD 21202 | Simu: (410) 528-1840 | Simu bila malipo katika jimbo la Maryland 1-877-261-8807 | Faksi: (410) 576-6571 | Barua pepe: heau@oag.state.md.us
- Hati za rufaa zilizo katika data na mfumo wa kazi wa mhusika wa tatu zitapitiwa na daraja la usimamizi linalofuata ambalo liko juu ya mwakilishi aliyekataa ombi la kwanza.
- Kuwasilisha barua ya uamuzi wa mwisho kwa kila mgonjwa ambaye amewasilisha rufaa rasmi.

<u>Kutolewa kwa Idhini ya Hali ya Kifedha na Kubatilishwa kwa Maamuzi Kunakochangiwa na Madaktari</u>

Katika hali ambapo kuna manufaa muhimu sana ya elimu, matibabu, na/au kihisani, madaktari wa UMMS wanaweza kuomba kutolewa kwa idhini ya hali ya kifedha kwa ajili ya wagonjwa wasio na uwezo au uwezekano wa kulipia huduma zao za matibabu. Wafanyakazi walio wataalamu wa matibabu sharti wawasilishe sababu kamili inayopaswa kutolewa kabla ya mgonjwa kupata huduma. Ofisi kuu ya kuandaa na kutuma bili ya

UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **11 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

Duru ya Mapato ya UMMS itatathmini ustahiki wa mgonjwa wa kupata Bima ya Matibabu na msaada wa kifedha. Kamati Tendaji ya Kutoa Idhini ya Hali ya Kifedha katika daraja la shirika lililo mwanachama, iliyo na uongozi wenye wafanyakazi wa taaluma ya matibabu na kifedha, itaomba taarifa zilizowasilishwa na ofisi ya mtaalamu wa matibabu na ofisi kuu ya kuandaa na kutuma bili, na kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu ikiwa idhini ya hali ya kifedha itatolewa kwa kuzingatia kila hali husika.

Ikiwa wagonjwa watapata idhini ya hali ya kifedha, bado wanahitajika kukamilisha mchakato wa maombi ya msaada wa kifedha, na huenda wakafanyiwa uchunguzi wa ustahiki wa kudhaniwa, kama ilivyoelezwa katika sera hii.

V. Notisi ya Upatikanaji wa Msaada wa Kifedha

UMMS itaarifu wagonjwa, familia za wagonjwa, na wawakilishi walioidhinishwa kuhusu kupatikana kwa msaada wa kifedha kupitia notisi zinazotumwa kwa posta pamoja na Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha. Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha humjulisha mgonjwa kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha na mipango ya malipo, inajumuisha maelezo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS, hutoa maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha ombi la msaada wa kifedha, na inajumuisha maelezo ya haki na wajibu wa mgonjwa kuhusiana na bili za hospitali na kudaiwa kwa madeni chini ya sheria.

- UMMS itachapisha notisi za kupatikana kwa msaada wa kifedha katika kila chumba cha dharura cha hospitali ya UMMS (ikiwa kipo) maeneo ya kulaza wagonjwa, maeneo makuu ambayo wagonjwa hutembelea, pamoja na ofisi ya hospitali inayoshughulikia bili za wagonjwa. Notisi za upatikanaji wa msaada pia zitatumwa kwa wagonjwa pamoja na bili za mgonjwa huyo.
- Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha itatolewa kabla ya kulazwa na kabla ya kuruhusiwa kuondoka hospitalini kila wakati mgonjwa yuko hospitalini, pamoja na kila bili ya hospitali, na itatolewa bila malipo kwa wagonjwa wote watakaoiomba, kwa njia ya posta na kwenye chumba cha dharura (kama kipo) na maeneo ya kulaza wagonjwa.
- Sera ya Msaada wa Kifedha na fomu ya Maombi ya Msaada wa Kifedha pia itatolewa bila malipo kwa wagonjwa wote watakaoiomba, kwa njia ya posta na katika chumba cha dharura (kama kipo) pamoja na maeneo ya kulaza wagonjwa.
- Sera ya Msaada wa Kifedha, Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha, na fomu ya Maombi ya Msaada wa Kifedha pia itachapishwa wazi kwenye tovuti ya UMMS (www.umms.org).

<u>Maudhui ya Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha</u>

Kando na taarifa zilizorejelewa hapo juu, Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha pia itajumuisha:

- Tovuti na anwani za eneo/maeneo ambapo wagonjwa wanaweza kupata nakala za sera ya msaada wa kifedha na pia fomu ya maombi ya msaada wa kifedha
- Maagizo kuhusu jinsi ya kupata nakala ya sera ya msaada wa kifedha na pia fomu ya maombi ya msaada wa kifedha kwa njia ya posta bila malipo.
- Taarifa kuhusu upatikanaji wa tafsiri za hati za msaada wa kifedha.
- Maelezo ya mawasiliano ya Idara ya Huduma kwa Wateja Inayoandaa Bili ya Hospitali ya UMMS, ambayo iko tayari ili kumsaidia mgonjwa, familia ya mgonjwa, au mwakilishi wa mgonjwa aliyeidhinishwa ili aweze kuelewa bili yake, kuelewa haki na wajibu wa mgonjwa kuhusiana na bili hiyo, kufahamu jinsi ya kuwasilisha ombi la kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa, au

kujifunza jinsi ya kuwasilisha ombi la Bima ya Matibabu ya Maryland, au mipango mingine yoyote ambayo inaweza kumsaidia kulipa bili zake za matibabu.
- Maelezo ya mawasiliano ya Mpango wa Bima ya Matibabu wa Maryland.
- Arifa kwamba ada za daktari hazijajumuishwa kwenye bili ya hospitali na kwamba ada hizo hutozwa kando.
- Arifa inayojulisha wagonjwa kuhusu haki ya kuomba na kupokea kadirio la maandishi la jumla ya ada za huduma za hospitali zisizo za dharura, upasuaji, na bidhaa ambazo kwa kawaida zinatarajiwa kutolewa na hospitali kwa ajili ya huduma za kitaalamu.
- Arifa kwamba wagonjwa wanaostahiki kupata matibabu bila malipo au kwa gharama iliyopunguzwa huenda wasitozwe zaidi ya kiwango kinachotozwa kwa kawaida (AGB) kwa ajili ya huduma za dharura au matibabu yanayohitajika ili kutambua dalili au kutibu maradhi na majeraha.
- Sehemu inayomjulisha mgonjwa kuhusu uwezo wake wa kuwasilisha malalamiko rasmi katika tume ya HSCRC na pia katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ya Maryland.
- Sehemu ambayo mgonjwa ataweka herufi za kwanza za majina yake ili kuashiria kwamba amejulishwa kuhusu Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS

Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha itaandikwa kwa lugha rahisi, kama ilivyoelezwa na Masharti ya sheria ya 501(c)(3) Hospitali Zilizo Chini ya Sheria ya Matibabu ya Bei Nafuu – Kifungu cha 501(r), na itatolewa kwa lugha anayopendelea mgonjwa. Pia itakuwa na sehemu itakayowezesha wagonjwa kuweka herufi za kwanza za majina yao ili kuashiria kwamba wamefahamishwa kuhusu sera ya msaada wa kifedha.

VI. Hatua Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni

Masalio ya akaunti ambayo bado hayajalipwa huenda yakahamishwa na kuwa Madeni Yasiyotarajiwa Kulipwa (yanachukuliwa kama matibabu ambayo hayakulipiwa) na kutumwa kwa wakala ya nje ya ukusanyaji madeni au kwa mwanasheria wa UMMS kwa ajili ya shughuli ya kisheria na/au ya kukusanya deni. Wakala za mhusika wa tatu na/au wanasheria wanajukumika kwa pamoja na kwa kiasi kikubwa katika kutimiza masharti ya ukusanyaji madeni yaliyoorodheshwa katika sera hii, na pia katika Sera ya UMMS ya Mikopo na Ukusanyaji Madeni. Hatua za ukusanyaji madeni zinazofanywa kwa niaba ya UMMS na wakala ya ukusanyaji madeni au mwanasheria wa UMMS zinaweza kujumuisha Hatua zifuatazo Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni (ECA):

- Kutoa taarifa za sifa mbaya kuhusu mtu huyo kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo ya watu na biashara au mashirika yanayokusanya taarifa za mikopo za watu na biashara. UMMS haitatoa taarifa za sifa mbaya kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo kuhusu mgonjwa ambaye hakuwa na bima au aliyekuwa anastahiki kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa wakati wa huduma. UMMS haitatoa taarifa kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo hadi baada ya angalau siku 180 kutoka wakati bili ya kwanza ilitolewa. Kabla ya kutoa taarifa kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo, UMMS itabaini ikiwa mgonjwa huyo anastahiki kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa. UMMS haitatoa taarifa za sifa mbaya kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo kuhusu mgonjwa ikiwa UMMS ilifahamishwa na mgonjwa au kampuni la bima kwa mujibu wa sheria za nchi kwamba mchakato wa rufaa au mapitio ya uamuzi kuhusu bima ya matibabu unaendelea ndani ya siku 60 zilizotangulia, au ikiwa UMMS imekamilisha ombi la kubadilishwa kwa uamuzi wa

kumnyima mgonjwa matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa ambalo lilikamilishwa ipasavyo na mgonjwa ndani ya siku 60 zilizotangulia.

- Kuanzisha mchakato wa kesi ya madai dhidi ya mtu huyo. UMMS haitawekea mume/mke au mtu mwingine lawama kwa ajili ya deni la bili ya hospitali la mtu ambaye ana umri wa angalau miaka 18. UMMS haitawasilisha ombi la madai la kukusanya deni hadi baada ya angalau siku 180 kutoka wakati bili ya kwanza ilitolewa. Kabla ya kuwasilisha ombi la madai la kukusanya deni, UMMS itabaini ikiwa mgonjwa anastahiki kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa. UMMS haitawasilisha ombi la madai la kukusanya deni ikiwa UMMS iliarifiwa kwa mujibu wa sheria za taifa na mgonjwa au kampuni la bima kwamba rufaa au kupitiwa kwa uamuzi wa bima ya afya bado hakujakamilika, ndani ya siku 60 zilizotangulia. UMMS haitawasilisha ombi la madai la kukusanya deni ikiwa UMMS imekamilisha ombi la kubadilisha maamuzi kuhusu kumnyima mgonjwa matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa ambalo lilikamilishwa ipasavyo na mgonjwa ndani ya siku 60 zilizotangulia.
- Kuchukua umiliki au kuhamisha fedha za akaunti ya mdaiwa au mali nyingine ya binafsi ili kukusanya deni.
- Kutumia amri ya mahakama ili kukusanya deni kupitia mshahara wa mtu. UMMS haitaomba amri ya mahakama ya kukusanya deni kupitia mshahara wa mtu au kuchukua hatua inayoweza kusababisha kukatwa kwa mshahara wa mgonjwa ili kulipa deni ikiwa mgonjwa huyo anastahiki kupata matibabu bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa.

Hatua Zisizo za Kawaida za Kukusanya Madeni (ECAs) zinaweza kuchukuliwa kwa akaunti ambazo hazina migogoro au zisizo na mipango ya malipo. Hatua Zisizo za Kawaida za Kukusanya Madeni (ECAs) hazitachukuliwa kabla ya siku 180 kutoka siku ya kutolewa kwa bili ya kwanza kwa mgonjwa na itatanguliwa na notisi ya maandishi siku 45 kabla ya kuanzishwa kwa mchakato wa ECA. Notisi hii ya maandishi itaandamana na maombi ya msaada wa kifedha (pamoja na maagizo ya kukamilisha maombi hayo) na notisi kuhusu upatikanaji wa mpango wa malipo ili kulipa deni lililotokana na huduma za matibabu, na Hati ya Taarifa Kuhusu Bili za Mgonjwa na Msaada wa Kifedha. Notisi hiyo ya maandishi itakuwa na taarifa zifuatazo:

- Maelezo mahususi za mawasiliano na taratibu.
    - Jina na nambari ya simu ya UMMS,
    - Jina na nambari ya simu ya mkusanyaji madeni (ikiwa inatumika)
    - Maelezo ya mawasiliano ya Idara ya Msaada wa Kifedha ya UMMS (au wakala ya mshirika wa tatu inayofanya kazi kwa niaba ya UMMS), iliyopewa idhini ya kurekebisha masharti ya mpango wa malipo (kama inatumika)
    - Nambari ya simu na anwani ya intaneti ya Kitengo cha Elimu ya Afya na Utetezi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kilicho tayari kusaidia wagonjwa walio na madeni yaliyotokana na huduma za matibabu.
- Kiasi cha pesa kinachohitajika kulipa deni hilo (ikiwa ni pamoja na madeni ambayo muda wake wa kulipwa umepita, faini, au ada, kama inatumika)
- Kutambuliwa kwa hatua zisizo za kawaida za ukusanyaji madeni ambazo UMMS (au wakala yake ya ukusanyaji madeni au mwanasheria, au mhusika mwingine aliyeidhinishwa) inanuia kuchukua ili kupata malipo ya matibabu, na kutaja tarehe ambayo itakapopita, hatua hizo zitachukuliwa.
- Tarehe ambayo itakapopita, ECA za aina hiyo zinaweza kuchukuliwa baada ya siku 45 kutoka tarehe ya kutolewa kwa notisi ya maandishi.
- Taarifa inayopendekeza kwamba mgonjwa atafute huduma za ushauri kuhusiana na madeni,

- Maelezo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS pamoja na arifa kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha kwa watu wanaostahiki
- Na taarifa zingine zozote kulingana na maagizo ya HSCRC

Notisi ya maandishi na hati husika zitatumwa kwa mgonjwa kwa njia ya posta inayompa mtumaji ithibati ya kutumwa na kuwasilishwa kwa barua, na huduma ya posta ya daraja la juu, katika lugha anayopendelea mgonjwa, au lugha nyingine, kama ilivyoelezwa. Notisi hiyo ya maandishi itakuwa katika lugha iliyo rahisi kuelewa na yenye matini ya angalau ukubwa wa saizi ya 10.

Kando na hiyo taarifa ya maandishi, UMMS (na/au wakala yake ya ukusanyaji madeni au mwanasheria) itachukua hatua zote zinazowezekana ili kumjulisha mgonjwa kwa maneno kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha na kumwambia jinsi anavyoweza kupata usaidizi wakati wa mchakato wa kuwasilisha ombi. Mapitio ya ustahiki wa kudhaniwa kabla ya uamuzi wa ustahiki kamili yatafanywa kabla ya Hatua zozote Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni kuchukuliwa. Mwishowe, Hatua Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni zitakazoanzishwa hadi wakati idhini itakapotolewa na uongozi wa Huduma za Duru ya Mapato katika UMMS.

Ikiwa itabainiwa kwamba mgonjwa anastahiki kupata msaada wa kifedha, UMMS (na/au wakala yake ya ukusanyaji madeni au mwanasheria) itachukua hatua zote zinazowezekana ili kubatilisha hatua zozote zisizo za kawaida za ukusanyaji madeni zilizochukuliwa dhidi ya mgonjwa ili kupata malipo ya matibabu yaliyotolewa ndani ya kipindi cha ustahiki wa msaada wa kifedha. Hatua za aina hiyo zinazoweza kupatikana kwa urahisi zitakuwa ni pamoja na kubatilisha hukumu zozote dhidi ya mgonjwa, kuondoa ada au madai ya kumiliki mali ya mgonjwa, na kuondoa taarifa zozote za sifa mbaya kwenye ripoti ya mikopo ya mgonjwa ambazo zilitolewa kwa wakala zinazoweka ripoti za hali ya mikopo ya watu na biashara au mashirika yanayokusanya taarifa za mikopo za watu na biashara. Hatua zote Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni zitasimamishwa punde baada ya mgonjwa kuidhinishwa kupata msaada wa kifedha na masalio yote kulipwa ambayo mgonjwa huyo anafaa kulipa.

UMMS haitachukua Hatua Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji Madeni zifuatazo:

- Kuuza deni kwa mtu mwingine.
- Kutoza riba kwa bili za wagonjwa kabla ya hukumu ya mahakama kupatikana
- Kuomba dai la kumiliki makazi ya msingi ya mgonjwa hadi deni litakapolipwa. Katika hali zingine, itifaki za Eneo, Jimbo, au Taifa zinaweza kuamuru kwa dai la kumiliki mali litolewe, lakini UMMS haitalazimu mgonjwa kuuza makazi yake ya msingi au kuchukua umiliki wa makazi ya mgonjwa ya msingi yanayolipiwa rehani.
- Kuomba kutolewa kwa, au kuchukua hatua itakayosababisha mahakama kumtia nguvuni mgonjwa au kutoa kibali cha kumtia nguvuni mgonjwa.
- Kuwasilisha dai dhidi ya mali ya mgonjwa aliyefariki ikiwa mgonjwa huyo aliyefariki alikuwa amebainishwa na UMMS kwamba anastahiki kupokea matibabu bila malipo au ikiwa thamani ya mali hiyo baada ya kutoa ushuru iko chini ya nusu ya deni analodaiwa. Hata hivyo, UMMS inaweza kupatia familia ya mgonjwa aliyefariki nafasi ya kuomba msaada wa kifedha.
- Kuhitaji malipo ya deni la huduma za matibabu kabla ya kutoa huduma zinazohitajika ili kutambua magonjwa au kutibu magonjwa na majeraha.

UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **15 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

VIAMBATISHO:

KIAMBATISHO CHA A: Gharama Inayobadilika Kulingana na Mapato – Gharama ya Matibabu Iliyopunguzwa

Ukubwa wa Kaya	1	2	3	4	5	6	Tazama Vikomo vya Msaada wa UMMS hapa chini
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$14,580	$19,720	$24,860	$30,000	$35,140	$40,280	

Miongozo ya Vikomo vya Ustahiki wa Mapato ya Mwaka ya vya Maryland Dept of Health (MDH) 2022							
Ukubwa wa Kaya	1	2	3	4	5	6	Tazama Vikomo vya Msaada wa UMMS hapa chini
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$20,120	$27,225	$34,312	$41,400	$48,504	$55,592	

Vikomo vya Mapato vya Kustahiki Kupata Msaada wa Kifedha wa UMMS							
Ikiwa jumla ya mapato ya mwaka ya kaya (HH) yako ni ya kiasi cha au chini ya:							Unastahiki kupokea msaada wa kiwango kifuatacho kutoka kwa UMMS:
Ukubwa wa Kaya	1	2	3	4	5	6	
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$40,240	$54,450	$68,624	$82,800	$97,008	$111,184	**Msaada wa 100%** (Sawa na 200% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$42,252	$57,173	$72,055	$86,940	$101,858	$116,743	**Msaada wa 90%** (Sawa na 210% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$44,264	$59,895	$75,486	$91,080	$106,709	$122,302	Msaada wa 80% (Sawa na 220% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$46,276	$62,618	$78,918	$95,220	$111,559	$127,862	**Msaada wa 70%** (Sawa na 230% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$48,288	$65,340	$82,349	$99,360	$116,410	$133,421	Msaada wa 60% (Sawa na 240% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$50,300	$68,063	$85,780	$103,500	$121,260	$138,980	**Msaada wa 50%** (Sawa na 250% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$52,312	$70,785	$89,211	$107,640	$126,110	$144,539	**Msaada wa 40%** (Sawa na 260% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$54,324	$73,508	$92,642	$111,780	$130,961	$150,098	**Msaada wa 30%** (Sawa na 270% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$56,336	$76,230	$96,074	$115,920	$135,811	$155,658	**Msaada wa 20%** (Sawa na 280% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)
Kikomo cha Mapato (kiwango cha juu zaidi)	$58,348	$78,953	$99,505	$120,060	$140,662	$161,217	**Msaada wa 10%** (Sawa na 290% ya vikomo vya Mapato ya Kila Mwaka vya MDH)

*Mapunguzo yote yaliyotajwa hapo juu yatatumika kwa kiwango ambacho mgonjwa atawajibika kufanya malipo yeye binafsi baada ya kurejeshewa gharama na bima.

*Kiasi cha bili ya wagonjwa wanaostahiki kupata Matibabu Yenye Gharama Iliyopunguzwa kulingana na mapato (au kwa ajili ya Msaada wa Matatizo ya Kifedha) kitakuwa chini ya kiasi cha bili cha watu wenye bima (AGB), ambacho katika jimbo la Maryland, ndicho kiwango cha ada kilichowekwa na Tume ya Mapitio ya Gharama za Huduma za Afya (HSCRC). UMMS huamua kiwango cha AGB kwa kutumia kiwango ambacho Medicare inaweza kuruhusu kutumika kwa ajili ya matibabu hayo (pamoja na kiwango ambacho mnufaishwa atawajibika kulipa mwenyewe, ambacho ndicho kiasi cha HSCRC; hii inajulikana kama "mbinu ya matazamio ya Medicare".

Itaanza Kutumika Mnamo 07/01/23

UNIVERSITY of MARYLAND MEDICAL SYSTEM **Huduma za Duru ya Mapato**	**UKURASA:** **16 KATI YA KURASA 16**	**NAMBARI YA SERA:** **RCS - 01**
	TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA: 09/18/19	**TAREHE ZA MARUDIO:** 07/01/23
MAUDHUI: Sera ya Msaada wa Kifedha ya UMMS		

SERA ZINAZOHUSIANA:
Sera ya Mikopo na Ukusanyaji Madeni ya UMMS
Sera ya Mipango ya Malipo ya UMMS

MMILIKI SERA:
Huduma za Duru za Mapato za UMMS

ILIIDHINISHWA:
Kamati Tendaji ya Utiifu Iliidhinisha Sera ya Kwanza: 09/18/19
Kamati Tendaji ya Utiifu Iliidhinisha Marekebisho: 10/19/2020, 11/07/22

Kiwango cha Umaskini cha Serikali ya Taifa na Maryland Department of Health Kikomo cha Ustahiki wa Mapato kwa Mwaka Kilisasishwa: 07/01/20, 07/01/21, 07/01/22, 07/01/23

Sera hii iliidhinishwa na Bodi ya Kamati Tendaji ya Utiifu ya UMMS (ECC) mnamo Oktoba 19, 2020. Sera hii ilirekebishwa kwa ajili ya:

- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland cha St. Joseph (UMSJMC) na ilianza kutumika mnamo Juni 1, 2013.
- Kampasi ya Midtown ya Chuo Kikuu cha Maryland (MTC) na ilianza kutumika mnamo Septemba 22, 2014.
- Kituo cha Matibabu cha Baltimore Washington cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMBWMC), na ilianza kutumika mnamo Julai 1, 2016.
- Kituo cha Matibabu cha Eneo la Pwani cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMSRH), na ilianza kutumika mnamo Septemba 1, 2017.
- Kituo cha Matibabu cha Mkoa cha Charles cha Chuo Kikuu cha Maryland (UMCRMC), na ilianza kutumika mnamo Desemba 2, 2018.
- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland cha Upper Chesapeake (UCHS), na ilianza kutumika mnamo Julai 1, 2019
- Kituo cha Matibabu cha Chuo Kikuu cha Maryland cha Mkoa wa Capital (UMCRH), na ilianza kutumika mnamo Septemba 18, 2019